TANGAZO LA SERIKALI Na. 39 la tarehe 24/02/2017.

SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
SURA YA 288

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 89*

SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI BIASHARA YA MAZAO YA MISITU) HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA ZA MWAKA, 2017

| | | |
|---|---|---|
| Jina la tarehe ya kuanza kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Udhibiti Biashara ya Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga, za Mwaka, 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. |
| Eneo la kutumika | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga. |
| Tafsiri | 3. | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:- |

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Mafinga;

"Mazao ya Misitu" maana yake ni mbao, nguzo ndogo (Milunda) ,nguzo kubwa, mkaa, fito na magogo mabichi na makavu;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;'

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi au Shirika ambalo linanunua mazao ya Misitu ndani ya Halmashauri na itahusisha pia mtu, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi au Shirika ambalo linasafirisha mazao nje ya Halmashauri.

"Muuzaji" maana yake mtu, Kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi au shirika lolote linalojishughulisha na uzalishaji au uuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri'

"Serikali ya kijiji" maana yake ni mamlaka ya kijiji iliyopo ndani ya mamlaka ya Halmashauri na ambapo mazao ya misitu yanauzwa na kununuliwa.

"Ushuru" maana yake ni ushuru wa mazao ya misitu usiozidi asilimia 5 ya bei ya kununulia kwenye chanzo unaolipwa na mnunuzi kwa Halmashauri pamoja na ushuru wa huduma unaolipwa kwa Halmashauri na muuzaji wa mazao ya misitu kutokana na asilimia 0.3 ya mauzo ya biashara husika.

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi, Shirika au Serikali ya Kijiji atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi'

Uanzishaji wa utaratibu maalum wa uuzaji na ununuziwa mazao ya misitu

4. (1) Halmashauri imeanzisha utaratibu maalumu wa uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu yanayopatikana ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mazao ya misitu yatauzwa, kununuliwa na kutozwa bei kwa kutumia kipimo cha mita za ujazo.

(3) Kila muuzaji na mnunuzi wa mazao ya misitu anawajibika kuuza au kununua mazao ya misitu na kutoza bei ya zao husika kwa kutumia kipimo cha mita za ujazo.

(4) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Kila zao la misitu litauzwa, kununuliwa na kutozwa bei yake kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo.

Wajibu wa Mnunuzi wa mazao ya misitu

5. (1) Utakuwa ni wajibu wa kila Mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri kununua mazao yake na kulipa malipo yake kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo kwa kila zao atakalonunua ikiwa ni pamoja na kulipa ushuru unaostahili kwa Halmashauri;

(2) Ni kosa kwa Mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri kununua mazao ya misitu kinyume na utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 5(1);

Wajibu wa Muuzaji wa mazao ya misitu

6. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kila Muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri anao wajibu wa kuhakikisha anauza na kutoza bei ya mazao yake ya misitu kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo ikiwa ni pamoja na kulipa ushuru unaostahili kwa Halmashauri;

(2) Kila Muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri atawajibika kuhakikisha anatoa taarifa katika Ofisi ya Kijiji mara atakapoona mtu yeyote anauza au kununua mazao ya misitu kinyume na utaratibu ulioelezwa na Sheria Ndogo hizi;

Leseni ya biashara ya mazao ya misitu

7. (1) Kila Muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri analazimika kuwa na leseni ya kuendesha biashara ya mazao ya misitu.

(2) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, leseni ya usajili wa biashara ya mazao ya misitu itakuwa ni lazima kwa kila muuzaji wa mazao ya misitu ikiwa ni pamoja na mtu yeyote anayeuza mazao hayo kutoka shambani kwake.

(3) Ni kosa kwa Muuzaji yeyote wa mazao ya misitu kuendesha biashara hiyo bila kuwa na leseni ya usajili wabiashara ya mazao ya misitu na leseni ya biashara ya mazao ya misitu kutoka Halmashauri.

Ushuru

8. (1) Utakuwa ni wajibu kwa kila muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri kulipa ushuru wa huduma

wa asilimia 0.3 ya mauzo ya mazao yake bila VAT.

(2) Ushuru unaolipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) hapo juu,ni kutokana na muuzaji kuendesha biashara ya mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(3) Utakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri kulipa ushuru wa mazao ya misitu usiozidi asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia.

(4) Katika kudhibiti ukwepaji wa ulipaji Ushuru, bei ya soko ya wakati huo itatumika katika kukokotoa ushuru anaotakiwa kulipa Mnunuzi wa mazao ya misitu.

(5) Ushuru utalipwa kwa Afisa muidhiniwa au wakala na muuzaji au mnunuzi wa mazao ya misitu kabla ya mnunuzi wa mazao kusafirisha mazao husika na kupewa stakabadhi ya Halmashauri

Wajibu wa Serikali ya Kijiji

9. (1) Utakuwa ni wajibu wa kila Serikali ya Kijiji ndani ya mamlaka ya Halmashauri kuhakikisha inatoa vibali vya uvunaji na ununuzi wa mazao ya misitu kwa kila muuzaji na mnunuzi ndani ya Kijiji husika;

(2) Utaratibu wa utoaji wa vibali vya uvunaji na ununuzi wa mazao ya misitu ndani ya Kijiji utakuwa ni wa lazima kwa kila muuzaji na mnunuzi.

(3) Kila muuzaji na mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya Kijiji atalazimika kupata kibali cha uvunaji na ununuzi wa mazao ya misitu katika Ofisi ya Kijiji kama ilivyoelezwa katika Fomu namba 1 na namba 2 za Sheria Ndogo hizi.

(4) Serikali ya Kijiji inaweza kufuatilia na kujiridhisha endapo muuzaji au mnunuzi wa mazao ya misitu aliyepewa kibali cha ukataji au ununuzi wa mazao ya misitu anazingatia matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa Wakala/ Afisa muidhiniwa

10. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumteua Wakala au Afisa muidhiniwa kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

(2) Wakala au Afisa muidhiniwa atakayeteuliwa na

Halmashauri atakuwa na jukumu la kuhakikisha matakwa ya Sheria Ndogo hizi yanatekelezwa na kutoza faini kwa niaba ya Halmashauri kama ilivyoelezwa na Sheria Ndogo hizi;

Viwango vya bei za uuzaji mazao

11. (1) Bila kuathiri masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi, bei za uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu itatozwa kwa kipimo cha mita za ujazo kwa kila aina ya zao la msitu;

(2) Bei ya uuzaji na ununuzi wa kila zao la misitu itatozwa na kubadilika kulingana na hali halisi ya soko la zao husika.

(3) Bila kuathiri masharti yaliyotajwa katika kifungu cha 11(1) na (2) hapo juu, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu na vyama vya wakulima wa miti inaweza kutoa bei elekezi ya uuzaji na ununuzi mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri bila kumwathiri muuzaji na mnunuzi wa zao husika.

Uanzishwaji wa Vituo vya ukaguzi wa Mazao ya Misitu

12. (1) Halmashauri inaweza kuanzisha Vituo mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya kukagua mazao ya misitu yanayosafirishwa kutoka ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Ukaguzi wa mazao ya misitu Vituoni utahusisha uhakiki wa nyaraka za uuzaji na ununuzi wa zao husika, ushuru uliolipwa ikiwa ni pamoja na bei ya kununulia na vibali vilivyotolewa Kijijini kuruhusu uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu.

Usafirishaji wa mazao ya misitu

13. (1) Kila msafirishaji wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri atahakikisha anapata nyaraka muhimu za mzigo wake kama ifuatavyo:-

a) Vibali vya uvunaji wa mazao ya misitu vilivyotolewa na Kijiji kwa muuzaji na mnunuzi wa zao hilo,
b) Nyaraka zinazoonyesha bei iliyotumika kununua zao husika kwa vipimo vya mita za ujazo,
c) Kibali cha kusafirisha zao husika.
d) Nakala ya stakabadhi ya ushuru uliolipwa na

muuzaji au mnunuzi wa mazao hayo.

e) Leseni ya usajili wa biashara ya mazao ya misitu.

f) Leseni ya biashara ya mazao ya misitu kutoka Halmashauri.

(2) Muda wa kusafirisha mazao ya misitu itakuwa ni kati ya saa 12:00 asubuhi na saa 12:00 jioni na si zaidi ya hapo.

(3) Ni kosa kwa msafirishaji yeyote wa zao la misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri kusafirisha zao lake bila kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(1) na (2) hapo juu.

Kutaifisha

14. (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kutaifisha na kuuza mazao ya misitu yaliyouzwa au kununuliwa bila kufuata masharti ya Sheria Ndogo hizi, endapo tu itaomba na kupata kibali cha Mahakama kwa madhumuni hayo.

(2) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea kwa muuzaji au mnunuzi wa mazao ya misitu yaliyotaifishwa, kwa kutekeleza mamlaka yake ya kuuza mazao hayo, endapo itakuwa imefuata masharti na utaratibu wa kuuza kama yalivyowekwa na Sheria ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini (50,000/=) mtu yeyote yule endapo mkosaji, atakiri kosa lake kwa maandishi kwa kujaza fomu namba 3 ya Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini.

Makosa

16. Mtu yoyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

a) Atauza mazao ya misitu kinyume na Sheria Ndogo hizi,
b) Atanunua mazao ya misitu kinyume na Sheria Ndogo hizi,
c) Atasafirisha mazao ya misitu bila ya kuwa na nyaraka zilizoelezwa katika kifungu cha 13(1), (a) – (f),
d) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi,
e) Atakataa au kushindwa kutii maagizo ya Afisa Muidhiniwa au Wakala,
f) Atamzuia Afisa Muidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake,
g) Atatishia uhai wa wakala au Afisa Muidhiniwa wakati akitekeleza majukumu yake,
h) Atalazimisha kupita katika Vituo vya ukaguzi wa mazao yamisitu kwa nguvu bila kukaguliwa,
i) Siyo msemaji wa Halmashauri, atatangaza hadharani kuwazuia watu wengine wasitekeleze matakwa ya Sheria Ndogo hizi,
j) Ataendesha biashara ya mazao ya misitu bila kuwa na leseni ya usajili wa biashara husika
k) Ataendesha biashara ya mazao ya misitu bila kuwa na leseni ya biashara kutoka Halmashauri.
l) Atauza mazao ya misitu bila kulipa ushuru wa huduma wa asilimia 0.3 kwa Halmashauri,
m) Atanunua mazao ya misitu bila kulipa ushuru wa mazao ya misitu wa asilimia 5 kwa Halmashauri,
n) Atanunua, kuuza au kutorosha mazao ya misitu kwa madhumuni ya kukwepa masharti ya sheria Ndogo hizi,
o) Atasafirisha mazao ya misitu nyakati za usiku.
p) Atasafirisha mazao ya misitu bila kulipa ushuru.

Adhabu

17. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tshs; 50,000/=) au kifungo cha miezi isiyozidi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja;

FOMU NAMBA 1

SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA BIASHARA YA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA ZA MWAKA, 2017

KIBALI CHA KUVUNA MAZAO YA MISITU

*(Chini ya kifungu cha 9(3))*

1. Jina la Muuzaji/Mvunaji:_______________________________________________________
2. Anuani S.L.P___________mji/kijiji___________kitongoji_________________________
   Simu____________________
3. Mahali anapoishi Mji/Kijiji ________________ Kitongoji:_________________________
4. Aina ya zao analotaka kukata:__________________________________________________
5. Jina la Mnunuzi:_________________________Anuani__________________
6. Kiasi cha Mazao kichovunwa/uzwa:________________________________________
7. Namba ya leseni ya biashara ya mazao ya misitu_______________________

**MIMI________________________________________NAAPA / NATHIBITISHA kwamba** nitauza mazao yangu ya misitu Kwa kuzingatia matakwa ya **Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za halmashauri ya Mji wa Mafinga za Mwaka, 2017** kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo katika kutoza bei na sio Vinginevyo. Pia natambua kuwa kuuza mazao hayo kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi ni kosa na nastahili adhabu.

Saini ya Mwombaji:_____________________________________________________Alama ya dole gumba_________________________________

Tarehe ya kusaini kibali:_______________________________________________

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji:________________________________________

Saini ya Afisa Mtendaji:________________________________________________

Mhuri wa Mtendaji wa Kijiji:_________________________________________________________

FOMU NAMBA 2

SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA BIASHARA YA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA ZA MWAKA, 2017

KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO YA MISITU

*(Chini ya kifungu cha 9(3))*

1. Jina la Mnunuzi:_______________________________________________
2. Anuani S.L.P ___________ Mji/kijji ____________________ kitongoji______________ Simu ____________________
3. Aina ya zao analotaka kununua:_______________________________________
4. Jina la Muuzaji:____________________anuwani _________________
5. Kiasi cha Mazao kitachonunuliwa:______________________________________

**MIMI___________________________________________________NAAPA / NATHIBITISHA;** kwamba nitanunua mazao ya misitu kwa kuzingatia matakwa ya **Sheria Ndogo za ( Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga za Mwaka 2017** kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo katika kulipa bei na sio Vinginevyo. Pia natambua kuwa kununua mazao hayo kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi ni kosa na nastahili adhabu.

Saini ya Mwombaji:_______________________________________________________

Alama ya dole gumba la Mwombaji__________________________________________

Tarehe ya kusaini kibali:____________________________________________________

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji:______________________________________________

Saini ya Afisa Mtendaji:____________________________________________________

Mhuri wa Mtendaji wa Kijiji:_________________________________________________________

FOMU NAMBA 3

SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA BIASHARA YA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA ZA MWAKA, 2017
HATI YA KUKIRI KWA HIARI KUTENDA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 15)*

Mimi:__________________________nakiri mbele ya Bw/Bi:______________Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga kwamba mnamo tarehe:_______________ya mwezi_________mwaka___________nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu namba__________________cha **Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga, za mwaka 2017**.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ambacho ni Tshs_______________badala ya kupelekwa Mahakamani ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamalaka aliyopewa chini ya kifungu cah 15 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku ni kifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa **Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga**, za mwaka 2016.
Jina la Mkosaji:_________________________________saini_____________alama ya dole gumba ____________________________________tarehe_______________________________

**Mbele ya Shahidi:**

Jina:____________________________________Saini________________________Alama ya dole gumba:__________________________tarehe:______________________________________
Jina la Mkurugenzi:______________________________________________________________
Saini ya Mkurugenzi:_____________________________________________________________
Tarehe:_________________________________________________________________________
Mhuri:_________________________________________________________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika vilivyo tarehe **19 Aprili 2016** na ilibandikwa mbele ya:

SAADA S, MWARUKA,
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji wa Mafinga*

CHARLES JOHN MAKOGA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji wa Mafinga*

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.)
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*